## MKATABA WA KUPANGISHA NYUMBA

Mkataba huu umefanyika leo tarehe 03 Mwezi wa…02 mwaka 2020

**BAINA YA**

**WAKURU MUSIKA GUBANI** wa S.L.P………… Nansio Ukerewe (ambaye katika mkataba huu ataitwa **MWENYE NYUMBA**), kwa upande mmoja;

**NA**

**DAMUKA INVESTMENT COMPANY LIMITED** wa S.L.P 236 Mwanza (ambaye katika mkataba huu ataitwa **MPANGAJI**) kwa upande mwingine.

A: **KWA KUWA**: Mwenye nyumba ni mmiliki halali wa nyumba iliyopo kiwanja No. 130 Kitalu " D" eneo la Nansio Ukerewe, ndani ya manispaaa ya wilaya ya ukerewe Jijini MWANZA na angependa kuipangisha kwa Mpangaji .

**NA**

B: **KWA KUWA:** Mpangaji anapenda kupanga nyumba hiyo tajwa hapo juu Pamoja na mambo mengine kwa kulipa kodi na masharti mengie.

## HIVYO PANDE ZOTE MBILI ZIMEKUBALIANA KAMA IFUATAVYO

1. **Kwamba** mwenye nyumba amekubali kumpangisha mpangaji nyumba iliyotajwa katika aya 'A' hapo juu kwa muda wa miaka 5 (miaka mitano) tangu tarehe 03/02/2020 hadi tarehe 03/02/2025

2. **Kwamba**, mpangaji amelipa kodi ya nyumba hiyo kiasi cha fedha za kitanzania shilingi 11,000,000/= (Milioni kumi na moja tu) kwa miaka yote mitano ambapo ni sawa milioni 2,200,000/= ( milioni mbili na laki mbili) tu kwa kila mwaka.

3. **Kwamba,** matengenezo magodogo madogo juu ya nyumba husika yatakuwa juu ya mpangaji isipokuwa matengenezo makubwa yatakuwa juu ya mwenye nyumba. Hata hivyo mpangaji hapaswi kufanya chochote chenye kubadili sura ya nyumba hata kama ni kidogo kiasi gani bila ridha ya mwenye nyuba.

4. **Kwamba**, mpangaji atatakiwa kuiweka nyumba katika hali ya usafi na kwa uharibifu wowote unaosababishwa na yeye au wakala wake, gharama ya ukarabati italipwa na mpangaji na iwapo uharibifu utatokana na uchakavu wa nyumba gharama ukarabati zitalipwa na mwenye nyumba.

5. **Kwamba** ,Mpangaji atalazimika kulipa gharaa za umeme na maji kwa kadri ya matumizi yake kila mwezi muda wote wa upangajina kabla ya kuondoka / kusitisha mkataba atahakikisha amelipa gharama zoteza maji na umeme alizotumia.

Scanned with CamScanner

6. **Kwamba**, mwenye nyumba na ndugu zake wa karibu watakuwa na haki ya kuingia na kukagua nyumba wakati wa mchana. Kwa maneno mengine ndugu zake wa karibu watajumuisha mke, Watoto,kaka na rafiki wa karibu aliyeewa aliyepewa mamlaka hayona mwenye nyumba.

7. **Kwamba**, mpangaji hataruhusiwa kumpangisha mtu mwingne ila kwa ridhaa ya maandishi ya mwenye nyumba.

8. **Kwamba,** iwapo mpangaji anatimiza masharti ya upangaji, mwenye nyumba atamwacha huru bila bughudha ili afurahie upangaji wake.

9. **Kwamba**, kila upande utakua na haki kusitisha mkataba huu kwa kutoa notisi ya miezi mitatu (3), hata hivyo mkataba huu unaweza kusitishwa wakati wowote iwapo mapangaji atavunja masharti ya upangaji.

10. **Kwamba**, iwapo mpangaji atahitaji kundelea na upangaji wa nyumba hiyo baada ya muda wa miaka mitano aliyopanga kuisha, mkataba huu utahuishwa na mpangaji atatoa taarifa ya maandishi ya kuendelea kuwa mpangaji wa nyumba hiyo.

11.

**KAMA MAKUBALIANO:** Pande zote mbili zimekubaliana kwa kuweka sahihi kama ifuatavyo hapa chini:

Imewekwa sahihi na **WAKURU MUSIKA GUBANI**
Ambaye ametambulishwa kwangu na………
…………………………………………………
Ambaye namfahamu, leo hii tarehe…03…..
Ya mwezi wa……02………………. …2020

WAKURU H. MSIKA
……………………………
**MWENYE NYUMBA**

**MBELE YANGU:**
Jina SELINA RYOBA MAGOIGA……
Saini……[signature]……
Anwani……716 Mwanza……
Cheo……Wakili……

SELINA RYOBA MAGOIGA Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths P.O. Box 716, MWANZA

Scanned with CamScanner

Imewekwa sahihi na **DANIEL NAMULANDA (mkurugenzi)**Kwa niaba ya Damuka Investment Company Ltd ambaye ametambulishwa kwangu na ……………………………………………………
Amabye namfahamu, leo hii tarehe….03….
Ya mwezi wa………02………… …2020

………………………………
**MPANGAJI**

DAMUKA INVESTMENT COMPANY
P.O. BOX 2361
MWANZA-TANZANIA

**MBELE YANGU:**

Jina…SELINA RYOBA MAGOIGA………
Saini……………………………………
Anwani……716 Mwanza………………
Cheo……Wakili…………………………

SELINA RYOBA MAGOIGA
Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths
P.O. Box 716

Scanned with CamScanner